**Learning by Ear – Girls' Rights**

**Episode 02**

**Title: Female Circumcision - A story of Girls' Rights**

**Author: Njoki C. Muhoho**

**Editors: Andrea Schmidt, Katrin Ogunsade**

**Proofreading: Michael Lawton**

**Kisuaheli: Eric Ponda**

**Characters**

**SCENE 1: TEACHER MONA'S HOME**

| | | | |
|---|---|---|---|
| NARRATOR | - | 30s: | MALE |
| CIRO | - | 15: | FEMALE |
| CHEPTOO | - | 15: | FEMALE |
| TEACHER MONA | - | 35: | FEMALE |

**SCENE 2 FATUMA'S PARENTS HOMESTEAD**

| | | | |
|---|---|---|---|
| NARRATOR | - | 30s: | MALE |
| TEACHER MONA | - | 35: | FEMALE |
| ELDER JACOB | - | 60S | MALE |
| JANET | - | 30S | FEMALE |
| 3 - 4 ELDERS | - | MIXED GENDER, 40-70S | |

**SCENE 3 SCHOOL CLASSROOM**

| | | | |
|---|---|---|---|
| TEACHER MONA | - | 35: | FEMALE |
| CLASS | | MIXED GENDER 14-16 | |
| CIRO | – | 15: | FEMALE |

| | | | |
|---|---|---|---|
| CHEPTOO | - | 15: | FEMALE |
| NARRATOR | - | 30s: | MALE |

**SCENE 4: FATUMA'S PARENTS HOMESTEAD**

| | | | |
|---|---|---|---|
| CIRO | – | 15: | FEMALE |
| FATUMA | - | 14: | FEMALE |
| CHEPTOO | - | 15: | FEMALE |
| NARRATOR | - | 30s: | MALE |

**SCENE 5: JANET'S OFFICE**

| | | | |
|---|---|---|---|
| JANET | - | 30s | FEMALE |
| CHEPTOO | - | 15 | FEMALE |
| FATUMA | - | 14: | FEMALE |
| CIRO | – | 15: | FEMALE |

**SCENE 6 FATUMA HOMESTEAD**

| | | | |
|---|---|---|---|
| ELDER JACOB | - | 60S | MALE |
| JANET | - | 30S | FEMALE |
| NARRATOR | - | 30S: | MALE |

**SCENE 7: SCHOOL COMPOUND**

| | | | |
|---|---|---|---|
| CIRO | – | 15: | FEMALE |
| TEACHER MONA | - | 35: | FEMALE |
| FATUMA | - | 14: | FEMALE |
| CHEPTOO | - | 15: | FEMALE |
| NARRATOR | - | 30s: | MALE |
| CLASS | - | MIXED GENDER, 14-16 YEARS | |

INTRO

**1. MUSIC: THEME MUSIC**

2. **NARRATOR** Hujambo na karibu kwa makala ya pili kwenye mchezo huu wa Learning By Ear Noa Bongo Jenga Maisha yako kuhusu **'Haki za Wasichana'**. Katika kipindi kilichotangulia Ciro na Cheptoo wafanikiwa kumtorosha rafiki yao Fatuma kutoka chumbani mwake ambako amekuwa akizuiliwa na wazazi wake ili kuozwa kwa lazima. Ni wasichana wajasiri na marafiki wakubwa. Hatimaye wasichana hao pamoja na rafiki yao Fatuma wanaelekea moja kwa moja hadi nyumbani kwa Mwalimu wao Mona, kutafuta ushauri zaidi. Katika kipindi cha leo Wasichana hao wanakumbana na chagamoto nyingine.Tatizo la upashaji tohara miongoni mwa wasichana.Endelea kuwa nasi ufahamu mengi zaidi Wakati wasichana hawa wanapotafuta haki za Mtoto wa kike.

**SCENE 1: TEACHER MONA'S HOME**

**3. SOUNDS: RUSHING MULTIPLE PAIRS OF FEET. PANTING. SIGHING.**

**4. SFX: LOUD REPETITIVE KNOCK ON DOOR.**

**5. SFX: FATUMA CRIES STEADILY**

6. **CIRO** Mwalimu Mona, Mwalimu Mona! Fungua!, fungua mlango tafadhali!

7. **CHEPTOO** Fungua Mwalimu,ni dharura!

**8. SOUND: FATUMA CRIES LOUDER**

**9. SFX: HEAVY MOVEMENT. FURNITURE MOVES AND CRUSHES.**

10. **TEACHER MONA** Ni nani? mnataka nini?

11. **CIRO** Ni sisi hapa Mwalimu, wanafunzi wako Ciro, Cheptoo na Fatuma.

12. **TEACHER MONA** Muna tatizo gani? Nini kinachomleta hapa saa hizi?

13. **CHEPTOO** Ni Fatu... Anaolewa

**14. SFX: DOOR HATCH SOUND. DOOR OPENS.**

15. **TEACHER MONA** Eti nini? Fatuma anaolewa?

16. **CIRO** Tumemtorosha...kutoka kwa mumewe mtarajiwa.

17. **CHEPTOO** Mwalimu afadhali umpe hifadhi hapa nyumbani kwako.

18. **TEACHER MONA** Hee…, hii ndio maana Fatuma hakuhudhuria shule leo kwasabau anaozwa?

19. **CIRO** (INTERRUPTS) Kisha kwa Kibabu!

20. **TEACHER MONA** (WITH URGENCY) Piteni ndani. Nitaenda kuwaona wazazi wa Fatuma. Na msitoke hapa. Sawa??

**<u>SCENE 2: FATUMA'S PARENTS HOMESTEAD</u>**

**21. <u>SFX: FARM SOUNDS</u>**

**22. <u>SFX: TROUBLED MURMURING</u>**

23. **TEACHER MONA** (FIRMLY) Nimekuja hapa kumuona Baba Fatuma.

24. **ELDER JACOB** Nani anayemtaka? Wewe Mwanamke, kwani huoni tuna mazungumzo mazito hapa?

25. **TEACHER MONA** Mimi ni Mwalimu Mona. Mwalimu wa Fatuma. Na hapa nimeandamana na Afisa wa masuala ya jamii, anaitwa Janet.

| | | |
|---|---|---|
| 26. | **JANET** | Tunataka kumzungumzia suala la Fatuma na mipango yenu ya kutaka kumuoza. |
| 27. | **ELDER JACOB** | Sasa munataka nirejesha Ng'ombe 50 niliochukua kama mahari? Fatuma atakuwa Mke mzuri sana kwa huyu Mzee mwenzangu... ni… |
| 28. | **JANET** | Tosha, tosha Mzee! Wasichana wadogo si mali ya Mnada. Fatuma ana haki ya kuendelea na masomo yake ili kuwa na maisha mazuri baadaye. Atakapo kuwa Mtu mzima, na pindi atakapokuwa tayari, bila shaka ataolewa na mume wa chaguo lake…. |
| 29. | **ELDER JACOB** | Mimi ndie Mzee wa boma hili, na sitaki ushauri wenu. |
| 30. | **JANET** | Hatukuja hapa kukwambia unachopasa kufanya, ibali kukuelimisha na pia kukukumbusha sheria zinazowalinda watoto.Fatuma ni mtoto mdogo sana, na ni hatia kumuozesha mapema. |

31. **ELDER JACOB** (ANGRY) Sasa kutokana na nuksi zenu, tumeahirisha mipango hiyo. Fatuma mwenyewe hayuko tayari kuolewa wakati huu,kwana ni lazima apashwe tohara. Na ndio mjadala unaoendelea hapa kwa hivi sasa.

32. **TEACHER MONA/JANET** Eti nini???

33. **ELDER JACOB** Nadhani sasa muda wenu umekwisha. munaweza kuondoka!

34. **NARRATOR** Mwalimu Mona na Afisa Janet wanafahamu kwamba tatizo hilo ni kubwa zaidi kuliko lile lililowapeleka..Babake Fatuma ana njama kubwa dhidi ya Fatuma. Je atatimiza lengo lake? Na je Fatuma atapashwa tohara? Upashaji tohara au Ukeketaji ni kukata sehemu nyeti za mwanamke, na mara nyingi huwa na athari za kiafya kwa mhusika.

Mwalimu Mona na Janet wanaondoka nyumbani kwa kina Fatuma lakini wasi wasi tatizo bado liko. Kwa kauli moja wanakubaliana kumlinda Fatuma dhidi ya njama hizi.

**SCENE 3: SCHOOL CLASSROOM.**

**35. SOUND: STUDENTS MURMURING**

**36. SFX: FURNITURE MOVEMENTS AS STUDENTS FIND THEIR SEATS**

| | | |
|---|---|---|
| 37. | **TEACHER MONA** | Habari za asubuhi wanafunzi. |
| 38. | **CLASS** | Ni nzuri Mwalimu Mona. |
| 39. | **TEACHER MONA** | Leo tutazungumiza haki zenu za msingi kuhusu elimu. Kumbuka nyote muna haki ya kupata elimu na wazazi wenu wanawajibu wa kuhakikisha kuwa mnapata elimu hiyo. |
| 40. | **CIRO** | Cheptoo ana bahati, Mamake aliajiriwa kama Mpokezi wa wageni katika Hoteli moja Mjini. |
| 41. | **CHEPTOO** | (SMUGLY) Hata mimi pia nataka kufanya kazi huko. Kwanza ukiona Hoteli yenyewe… ni … |
| 42. | **TEACHER MONA** | (VERY STERN) Sawa. Tosha basi. Lakini kwanza nilazima ukamilishe masomo yako. Nimesemaje wanafunzi? |
| 43. | **STUDENTS** | Kwanze tukamilishe masomo. |

| | | |
|---|---|---|
| 44. | **CHEPTOO** | (SMUGGLY) Mwalimu Mona lakini sihitaji Digrii ili kuwa Mpokezi wa wageni katika hoteli kubwa ya kifahari.Tayari elimu niliyoipata, ukichanganya na urembo wangu,..inatosha!. |
| 45. | **TEACHER MONA** | Cheptoo ukiwa na elimu nzuri, unaweza hata kuwa Meneja wa Hoteli hiyo. Au ungependa kufanya kazi hiyo tu kama mpokezi wa simu? |
| 46. | **CHEPTOO** | Hata kama usemavyo,ningependa kuwa Meneja. |
| 47. | **TEACHER MONA** | Sawa.Lakini endapo utaolewa mapema au kupashwa tohara na kufanya kazi badala ya kusoma, basi ufahamu ni kosa na kutaathiri maisha yako siku za usoni. Jambo kama hilo likitendeka njoo kwangu au kwa afisa wa jamii.<br><br>Lakini, Fatuma yuko wapi? Nani ameonana na Fatuma hivi punde? |
| 48. | **NARRATOR** | Ciro na Cheptoo wanawasi wasi kuhusu Fatuma. Na wanaamua kufunga safari kwenda kumtembelea tena nyumbani kwao. Hebu tuungane nao ili kufahamu zaidi yanayomsibu Fatuma. |

**<u>SCENE 4: FATUMA'S HOMESTEAD</u>**

**49. <u>SFX: FARM NOISES</u>**

50. **<u>SOUNDS: A LOT OF MURMURING</u>**.

| | | |
|---|---|---|
| 51. | **CIRO** | Fatuma… Fatuma...Unafanya nini nyumbani.Tulifaulu kusimamisha ndoa yako ya lazima na mbona hujafika shule leo? |
| 52. | **FATUMA** | (EXCITED) Oh, Wazazi wangu wanasema nimekuwa msichana mkubwa sasa.Japo sitaolewa wakati huu, lakini wakati utakapofika, lazima niwe Mwanamke aliye mkamilifu. |
| 53. | **CHEPTOO** | (SARCASTIC)Kwani sasa si mkamilifu? |
| 54. | **FATUMA** | Cheptoo, wewe unaishi Mjini , hufahamu vyema mambo ya kijijini. Wasichana wote wa rika langu lazima wapashwe tohara ili wawe wakamilifu. |
| 55. | **CHEPTOO** | Unaamanisha kukatwa sehemu zako za za siri. Huo ni ukatili!. |

| | | |
|---|---|---|
| 56. | **FATUMA** | Hapana… Nadhani hamunielewi. Huu ndio utamaduni wetu. Mamangu,na Dada zangu wote walipitia njia hiyo hiyo.Na sasa ni wakati wangu. Wasichana wote wa rika langu watapashwa tohara wiki hii. |
| 57. | **CHEPTOO** | Fatuma,wewe ni rafiki yetu, na huwezi kupitia haya yote. |
| 58. | **FATUMA** | Si nyinyi munao amua!.Ni lazima nipashwe tohara la sivyo linatalaniwa na kutengwa katika jamii.Nitachekwa!. |
| 59. | **CIRO** | Lakini hiyo isiwe sababu ya kupitia uchungu wote huo mbali na kuhatarisha afya yako. |
| 60. | **CHEPTOO** | Fatuma,nina wazo. Kesho twende kwa Janet yule afisa wa masuala ya Jamii.Akisema ni sawa basi hakuna shida.Sisi hatutakusumbua tena. |

61. **NARRATOR** Fatuma binti mchapa kazi, kwa mara nyingine yumo mashakani.Ukosefu wa ufahamu ndilo tatizo lake kubwa. Je ni vipi watamshawishi rafiki yao kwamba ingawa utamaduni huu unaungwa mkono na wazazi wao, unaathari kubwa kwa afya yake? Na je ni vipi Fatuma ataweza kumudu hali hii?. Endelea kuwa nasi upate kujua yaliyojiri katika ofisi ya Janet,afisa wa masuala ya jamii.

**SCENE 5: JANET'S OFFICE**

62. **JANET** Ehhe wasichana, nimsaidie vipi?

63. **CHEPTOO** Fatuma anataka kupashwa tohara!

64. **FATUMA** Cheptoo, kwani umeambia utangaze?

65. **CIRO** Ehhhhh kama umekubali kuweka wazi uchi wake na katwa sehemu ya siri, pia mimi sina budi kuweka wazi suala hili.

66. **FATUMA** Bi Janet, hebu waeleze tafadhali...

67. **JANET** Sawa. Fatuma, huwezi kuendelea na mipango hiyo ya kupashwa tohara.

68. **FATUMA** Kwanini? Ni wajibu wangu.

69. **JANET** Ni sawa, kwani kufanya hivyo utakuwa unatekeleza haki yako ya kimsingi.Lakini ingawa hizi ni tamaduni zetu ufahamu zimepitwa na wakati na baadhi yazo zinapasa kuchunguzwa upya hasa hii ya ukeketaji.

70. **FATUMA** Lakini wazazi na jamaa zangu hawafahamu hilo.

71. **JANET** Basi nitakuja kuzungumza na wazazi wako. Fatuma hii si kwamba ukikataa kukeketwa utalaaniwa au kutengwa na jamii, bali utakuwa mfano bora kwa wasichana wengine wa rika lako. Yaani kiongozi wa kutetea haki za wasichana.

Sasa ni lini tunaweza kuja kuzungumza na wazazi wako?

**<u>SCENE 6: FATUMA PARENTS' HOME</u>**

**72. <u>SFX; FARM SOUNDS.</u>**

| | | |
|---|---|---|
| 73. | **ELDER JACOB** | Wewe si yule afisa mpelelezi wa masuala ya jamii, Janet,sivyo? |
| 74. | **JANET** | Nafurahi bado wanikumbuka Mzee Jacob. Kilicho nileta hapa ni kuhusuj bintiyo Fatuma. |
| 75. | **ELDER JACOB** | Kulikoni tena?. Mliita doa ndoa ya binti yangu, na kunikosesha utajiri wa Ng'ombe nyingi tu. Sasa kilichokuleta hapa ni nini? |
| 76. | **JANET** | Hujapoteza chochote Mzee Jacob, bali utakuwa na binti mzuri mwenye afya atakaye kuzalia watoto wakati utakapofika. Fatuma hapasi kupashwa tohara. |
| 77. | **ELDER JACOB** | Nani kasema hivyo! Huu ni utamaduni wetu tangu jadi. Binti yangu lazima apashwe tohara ili awe  Mwanamke mkamilifu.Katika ulimwengu huu ni lazima ujifunze yale yote wanawake wanayopasa kufahamu. Na yeye ana mengi  ya kujifunza kama Mwanamke. |

| | | |
|---|---|---|
| 78. | **JANET** | Nakubaliana nawewe Mzee Jacob. Wasichana wote wa rika lake wanawajibu wa kuifahamu vyema mili yao, afya na hata uhusiano wa kujinsia. |
| 79. | **ELDER JACOB** | (LAUGHING) Ehhheeee, sasa naona tutaelewana. Tayari kila kitu kimepangwa. |
| 80. | **JANET** | (LAUGHING)Hata mimi nafurahi kwamba tuko pamoja. Nasi pia mipango yetu yote imekamilika.Kila mwishoni mwa wiki tutakuwa tukiandaa vikao na wasichana wa rika la Binti yako Fatuma. Na wazungumzaji watajaribu kuwaelimisha wasichana kuhusu masuala ya wanawake.Vikao hivi vinaanza mwishoni mwa wiki hii. Hivyo hakiisha Fatuma anafika mapema kabisa. |
| 81. | **ELDER JACOB** | Eti nini?! |
| 82. | **JANET** | Katika mafunzo haya maalum, tunajadilia changamoto zinazowakumba wasichana katika jamii. |

83. **NARRATOR** Babake Fatuma huenda hatakubaliana na wazo la kutupilia mbali utamaduni huu, lakini msingi ni kwamba amefahamu kwamba zipo njia mbadala za wasichana kuvuka daraja hili pasi na kupashwa tohara.Amefahamu kwamba wasichana wanaweza kuwa wanawake wakamilifu bila ya kukektewa.Sasa shule na jamii nzima kwa jumla wataandaa vikao kwa wazee kuwahamasisha dhidi ya ukeketaji.

**<u>SCENE 7: SCHOOL COMPOUND</u>.**

**84. <u>SFX: SCHOOLROOM NOISES</u>**

85. **CIRO** Mwalimu Mona... ?

86. **TEACHER MONA** Naam Ciro?

87. **CIRO** Ama kwahakika naogopa kuwa msichana mkubwa. Zamani nilipokuwa mdogo mambo yalikuwa rahisi tu.

88. **TEACHER MONA** Usinichekeshe.Kwanini waogopa? Fatuma…, unasemaje?

| | | |
|---|---|---|
| 89. | **FATUMA** | (SADLY) Mambo haya sasa yameanza kunichanganya. Nataka sana kuwaheshimu wazazi wangu, tamaduni zetu, lakini kwa upande mwengine, nataka kufahamu zaidi haki zangu maishani … katika kila jambo. |
| 90. | **TEACHER MONA** | Na wewe Cheptoo, unasemaje? |
| 91. | **CHEPTOO** | (WITH BRAVADO). Ni rahisi sana Mwalimu. Wakati babangu aliponunua gari, lilikuja na stakabadhi zote za maelezo. Hivyo ni lazima tuelezwe tunachopasa kufanya na kile tusichopasa kufanya. Si hiyo itakuwa rahisi? |
| 92. | **ALL** | LAUGHTER |
| 93. | **CIRO** | Ni nawazo. Kwsnini tusianzishe chama cha wasichana ambapo tutakuwa na vikao kujadili masuala yanayotuhusu. Kila mmoja wetu anatoka katika mazingira tofauti. Cheptoo anaishi mjini, Fatuma kutoka kijijini, na mimi wazazi wangu hawajaona lango la darasa. |

94. **FATUMA** Vyema kabisa, na kwa hiyo tutaweza kubadilishana mawazo na kujadili masuala yanayogusia haki zetu.

95. **CHEPTOO** Lakini pia vilabu kama hivi hujihusisha na mambo mengi.. yaani shughuli za aina mbali mbali.. sasa sisi tutakuwa tukijihusisha na nini?.

96. **CIRO** Tutaandaa mijadala.

97. **CHEPTOO** Kama vile bunge... Hebu tulitafakari suala hili. Tunaweza kuunda bunge la wasichana.

98. **CIRO** (WITH GUSTO) Napendekeza darasa hili liunde bunge la wasichana.

99. **FATUMA** Na mimi naunga mkono.

100. **CIRO** Hoja imepitishwa. Sasa kuanzia leo sisi wasichana, tutakuwa tukukutana na kujadilia masuala mbali mbali yanayotuhusu hasa suala la haki zetu. Wale wanaounga mkono, waseme… ndio….

101. **CLASS** **(LOUDLY STAMPING FEET)** Ndio.. ndio… ndio…

**102. <u>THEME MUSIC</u>**

**OUTRO**

103. **NARRATOR** Bunge la wasichana sasa limeundwa. Wasichana hawa wamefahamu kwamba licha ya tofauti zao, wanakabiliwa na matatizo sawa kama vijana.Mwalimu Mona na afisa wa masuala ya jamii Bi Janet watawasaidia kuwapa habari muhimu mbali na kuingilia kati pingamizi zozote kutoka kwa wazazi wao wakati wa mijadala hiyo.Ungana na wasichana hawa katika kipindi kinachofuatia cha Noa bongo Jenga maisha yako ujifunze mengi zaidi'.

104. Pia unaweza kutembelea mtandao wetu wa www.dw-world.de/lbe kusikiza tena kipindi hiki au hata kutuma maoni yako.Usikose kuungana nasi tena wakati mwengine kwa kipindi kingine, kwaheri kwa sasall.